

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA THELATHINI NA SITA**

**27 MEI, 2019**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 27 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NISHATI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MADINI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Madini kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **297. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Mabweni katika Shule za Sekondari zilizoanzishwa Kitarafa ili kuwasaidia Watoto wa Kike waweze kupata elimu iliyo bora Mkoani Shinyanga.

#### **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

#### **298. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali iliahidi kuhamasisha Sekta Binafsi kuanzisha Viwanda vikubwa na vya kati na kuweka utaratibu wa kuvilinda dhidi ya Viwanda vya nje:-

- (a) Je, Serikali imefikia wapi katika azma hii ambayo ni mwelekeo wa kufikia uchumi wa kati na utoaji ajira hasa kwa Vijana;
- (b) Je, Serikali imeweka mkakati upi ili kuweza kujenga mazingira rafiki yatakayoweza kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji wa Viwanda.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**299. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Utalii wa baharini kupitia “*Diving*” unakua kwa kasi sana Duniani kote hali ambayo inaongeza soko la ajira katika Sekta hiyo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto za Soko la ajira kwa Vijana wa Kitanzania;
- (b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha usalama wa Watalii wanapokuwa chini ya maji hasa kutokana na uvuvi haramu wa kutumia mabomu.



## **WIZARA YA MADINI:**

### **300. MHESHIMIWA UPENDO FURAHA PENEZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-  
Wananchi wa Mtaa wa Mgusu wanaoishi ndani ya mipaka ya Mgodi wa *Geita Gold Mine* wanaathirika sana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka zinazomwagwa katika maeneo karibu na Wananchi:-

Je, ni lini Serikali itatoa agizo kwa *Geita Gold Mine* kulipa Wananchi fidia ili watoke katika eneo lililomilikishwa Mgodi.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **301. MHESHIMIWA SAUL HENRY AMON (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-  
Umeme wa REA umepita katika Vijiji vya Unyamwanga, Kisonidzela na Mpuga lakini Wananchi wa maeneo hayo hawajaunganishiwa huduma ya umeme:-

Je, ni lini Wananchi hao wataunganishiwa huduma ya umeme.

**302. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH  
BUKWIMBA (BUSANDA):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA III katika Kata za Bujula, Nyamalimbe, Kamena, Nyalwanzaja, Nyakamwaga, Busanda Kaseme, Magenge, Butindwe na Nyaruyeye.

**303. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA  
(MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA III katika Kijiji cha Hemsambia na Vitongoji vyake vyote.



**WIZARA YA KILIMO:**



**304. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU  
(HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-  
Serikali iliondoa kodi kwenye mbegu za Mahindi mwaka 2017 – 2018:-

Je, ni lini Serikali itasimamia upunguzwaji wa bei kubwa ya mbegu za Mahindi na pembejeo.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **305. MHESHIMIWA SAED AHMED KUBENEA (UBUNGO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Uvuvi katika nchi yetu ni shughuli inayohusu Wakazi wengi sana ikiwa ni ya pili kutoka kwenye Kilimo kwa kutoa ajira kwa Watanzania wengi:-

- (a) Je, ni lini na ni wapi Kiwanda cha Samaki kwa ukanda wa Pwani kitajengwa;
- (b) Je, mpango wa ujenzi wa Bandari ya Samaki umefikia wapi.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
27 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**